**Wamejipanga Dhidi Ya Mungu**

Shauku ya uhuru wa kuabudu imewapelekea wengi watoke katika mwambao Ulaya ya Magharibi kwenda kujaribisha mawimbi makali ya Antlantiki kwa ajili ya tumaini. Tumaini lilikuwa ni nchi ambayo mtu atamwabudu Mungu kwa uhuru. Nao wakaja Marekani, wakapigania uhuru. Na nchi hii kubwa ikapewa uhuru wa kuabudu.Sio tu kwamba uhuru wa kuabudu ulikuwepo, bali maadili ya kidini na dola kwa kiasi kikubwa yalifungamana. Msafara wa ugaidi Philadelfia na Washington D.C utathibitisha tu walichofikiria wahenga wetu kuhusu ukristo na nafasi yake katika Taifa letu!

Leo, kwa jina la uhuru wa kuabudu, bado, tangu bahari hadi bahari ing'arayo, mwanadamu anajaribu kulifuta Jina la Mungu. Kwa nini? "Kwanini mataifa wanafanya ghasia, na makabila wanatafakari ubatili?" Kwanini, "Wafalme wa dunia wanajipanga, na wakuu wanafanya shauri pamoja juu ya BWANA, na juu ya Masihi wake?" Zaburi 2:1-2. Sababu rahisi ni kwamba ufalme wa shetani haujafarakana, Mathayo 12:25ff.

Ndiyo, ninajua, Matendo ya Mitume 4:25-26 hutufundisha kwamba aya ya Zaburi 2 ilikuwa ni unabii kuhusiana na Yesu. Aya hii bado kwa namna ya pili huwafunda wakristo kwamba wasigutuke inapoonekana ulimwengu umeungana dhidi ya kazi ya Kristo. Hiyo ni kwa sababu, shetani, mkuu wa ulimwengu huu (Yohana 14:30), Hajafarakana, na kama alivyoitumia Rumi kujaribu kuusambaratisha ukristo, atatawala, na kuunganisha kila dola ya giza dhidi ya Kristo. Sasa, kwanini ACLU inaonekana kuwa dhidi ya Kristo? Kwa nini serikali yetu pole pole inaonekana kutunga sheria ili kupoka uhuru wetu wa kuabudu? Kwa nini dini kama Uislam na Ubudha wanapewa uhuru kwenye viwanja vingi kwa ajili ya mihadhara ndani ya Marekani? Kwa nini inaonekana baadhi ya mawakili wako tayari kupigania haki za Waislam na kugeuka kupigania kupoka haki ile ile kwa wale wanaomkiri Kristo kuwa ni Bwana?

Yawezekana yapo majibu mengi na sababu nyingi kwa ajili ya maswali hayo hapo juu. Lakini sababu kubwa ni kwamba leo shetani yuko vitani dhidi ya Yesu na kanisa lake, Ufunuo 12. Kwa hiyo, atatumia kila kilichoko kwenye ghala yake ili kutushitaki mbele za Mungu mchana na usiku, 12:10. Kwa kule kuwa mkuu wa ulimwengu huu, sehemu ya silaha zake ni kuunganisha maadui zetu kupigana nasi kwa masilahi ya kazi yake. Hivi, hukumkumbuki Pilato na Herode katika Luka 23:12? Walikuwa ni maadui hadi lini?

Haya yote yananikumbusha juu ya utekwaji wa Kanaani katika Kitabu cha Yoshua. Na katika Yoshua 9:1-2, twaweza kuona kuwa wafalme wote wa kusini mwa Kanaani waliungana ili kupigana na Israel. Hapo kabla, wafalme hawa walikuwa mahasimu waliokuwa wakipigana kila wakati kwa ajili ya ukanda wa juu. Walakini Mungu alipowaleta waisrael, Shetani aliwaunganisha waliokuwa maadui ili wapigane dhidi ya Mungu na wateule wake. Na leo, Jeshi la Mungu linatumia Injili kuuzingira ulimwengu, kuzikomboa nafsi zilizopotea, moja moja kwa ajili ya Mungu. Wamishonari wetu wanafanya kazi nzuri na makusanyiko yetu yako nyuma yao.

Kuzingira kunaendelea, na kwa mara nyingine tena, shetani anawaunganisha maadui ili kuzuia injili isisonge mbele!

Hivyo, uhuru wanaoufurahia wakristo Marekani utazidi kuzorota. Zipo jitihada za kufuta jina la Mungu kwenye kila kitu katika Dola yetu, kufuta jina lake kwenye kurasa za historia yetu. Wengine wanataka kuliondoa jina la Mungu kwenye viapo vyetu. Kuna jitihada zinafanyika za kuondoa misamaha ya kodi. Kuna jitihada za kufuta kila kipindi cha dini katika radio na luninga. Kwa madai kuwa mawimbi ya anga ni mali ya Dola, na hivyo wakristo wasiruhusiwe kuyatumia. Na haya yote ni sehemu tu ya vita.

Licha ya kujua yote haya, tusigutuke endapo kazi ya Kristo itazidi kuzorota hapa Marekani. Wakati huo huo, tusilegeze imani yetu maana kwa kule kujaribiwa kwa imani yetu tutapata sifa na heshima, 1 Petro 1:7. Tusiangalie nyuma maana anayegeuka kuangalia nyuma hafai katika ufalme wa Mungu, Luka 9:62. Tusiyumbe, na tuvumilie mabaya kama askari wema, 2 Timotheo 2:3. Na tukumbuke ya kuwa Yesu ameahidi kuwa na kanisa lake hata ukamilifu wa dahari, Mathayo 28:20. Hivyo, tukumbuke kuuangalia ule mji ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu, Waebrania 11:10. Kama kinavyofundisha kitabu cha ufunuo, bila kujali yanayotujia, tunaweza kushinda na TUTASHINDA!